

## SHULE YA AWALI, MWANZO MWEMA! **SWAHILI**



### NINI KINAWEZA KUTOLEWA NA SHULE YA AWALI?

- Katika shule ya awali, mtoto wako anaweza kucheza, kujifunza na kupata marafiki.
- Katika shule ya awali, lugha mbalimbali zinathaminiwa, na lugha ya Kinorejia inajifunzwa kuititia kushirikiana na wengine. Watoto wanawenza kujifunza lugha zaidi ya moja kwa wakati mmoja, na lugha ya mama yao inapaswa kuendeleza sambamba. Tunawahimiza wazazi kuzungumza lugha yao ya mama na watoto wao, kwani hii huunda msingi mzuri wa kujifunza baadaye. Wakati huo huo, lugha ya mama ni muhimu kwa maendeleo ya utambulisho wa mtoto.
- Mtoto atafahamiana na utamaduni wa Kinorejia na pia atapata fursa ya kushiriki utamaduni wao wenye. Kujifunza tamaduni za kila mmoja husaidia kuelewana kwa urahisi zaidi.
- Shule ya awali ni taasisi ya kielimu, ambayo ina maana kwamba mtoto hupata msaada katika michezo na shughuli mbalimbali ili aweze kupata uzoefu na kujifunza.
- Shule ya awali ni mwanzo wa elimu ya mtoto na huchangia katika kuweka msingi mzuri kwa ajili ya kuanza shule rasmi.
- Wakati mtoto wako yupo shulen, unaweza kujifunza Kinorejia, kwenda shule au kufanya kazi.

### JE, MTOTO WANGU YU SALAMA KATIKA SHULE YA AWALI?

Watoto wanatunzwa vyema na watu wazima wenye huruma na waliobobea katika kazi yao. Shule ya awali inafuata sheria na kanuni nyingi ambazo zinalenga kuhakikisha usalama wa watoto.

### NINAWEZAJE KUJUA KAMA MTOTO WANGU ANAFURAHIA KUWA KATIKA SHULE YA AWALI?

Wazazi na wafanyakazi wa shule ya awali wanashirikiana kwa kubadilishana taarifa kuhusu mtoto. Asubuhi, unaweza kueleza ikiwa mtoto amelala vizuri, amekula vya kutosha au ikiwa kuna jambo lolote maalum limetokea.

Hii inasaidia wafanyakazi kufanya siku ya shule ya awali kuwa bora zaidi kwa mtoto wako. Unapomchukua mtoto wako jioni, wafanyakazi watakueleza kile mtoto wako amefanya siku hiyo, kama vile chakula alichokula, michezo aliyocheza, au uzoefu alio nao. Unaweza pia kumuuliza mtoto wako akuonyeshe au akueleze. Ikiwa una wasiwasi au maswali muhimu, omba mazungumzo na mkalimani

### MTOTO WANGU ANAWEZAJE KUPATA NAFASI KATIKA SHULE YA AWALI?

Unaweza kuingia kwenye sehemu ya intaneti ya Manispaa ya Tønsberg na kutafuta sehemu iliyandikwa "**Barnehage**" kisha ubofye "**Her kan du søke om barnehageplass**" (Hapa unaweza kutuma maombi ya nafasi ya shule ya awali).

Ikiwa unahitaji msaada wa kupata nafasi, unaweza kwenda kwenye **Shule ya Awali ya Wazi (Åpen barnehage)**, ambayo iko wazi siku ya Jumatatu na Jumatano kuanzia saa 09:00 hadi 15:00.

Mahali: **Familiehuset, karibu na stesheni ya treni**  
Anwani: **Halfdan Wilhelmsens alle 2, 3116 Tønsberg**

### GHARAMA NI KIASI GANI?

- Ikiwa una kipato cha chini, unaweza kuwa na haki ya kulipa ada ya chini kwa shule ya awali.
- Ikiwa una watoto zaidi ya mmoja katika shule ya awali, una haki ya kulipa ada ya chini.

## BARNEHAGEN, EN GOD START!



### HVA KAN BARNEHAGEN BIDRA MED

- I barnehagen kan ditt barn leke, lære og få venner
- I barnehagen anerkjennes ulike språk og det norske språket læres gjennom å være sammen. Barn kan lære flere språk samtidig, og morsmål skal kunne utvikles parallelt. Vi oppfordrer foresatte til å snakke morsmål med sitt barn, det skaper en god basis for seinere læring. Samtidig er morsmål viktig for identitetsutviklingen.
- Barnet blir kjent med norsk kultur og får mulighet til å dele av egen kultur. Å bli kjent med hverandres kultur bidrar til at vi forstår hverandre lettere.
- Barnehagen er en pedagogisk institusjon det vil si at et barn i barnehagen på ulike måter får støtte i lek og aktiviteter for å kunne oppleve og lære.
- Barnehagen er starten på barnets utdanning og det bidrar til et godt grunnlag for å begynne på skolen
- Mens barnet er i barnehagen kan du for eksempel lære norsk, gå på skole eller jobb.

### ER BARNET MITT TRYGT I

#### BARNEHAGEN?

Barna blir tatt godt vare på av omsorgsfulle og kvalifiserte voksne.

Barnehagen følger mange lover og regler som skal gjøre barnehagen trygg.

### HVORDAN KAN JEG VITE OM BARNET MITTRIVES I BARNEHAGEN?

Foreldre og personalet deler informasjon om barnet. Om morgen kan du fortelle om barnet har sovet godt, om det har spist nok eller om det har det vært skjedd noe spesielt mm, da kan personalet bidra til at barnehagedagen blir best mulig. Når du henter ditt barn snakker de ansatte med deg om hva barnet for eksempel har erfart/spist/lekt denne dagen og sammen kan dere spørre barnet å vise/fortelle deg. Spør om en samtale med tolk hvis du er bekymret eller har viktige spørsmål.

### HVORDAN KAN MITT BARN FÅ EN PLESS I BARNEHAGEN?

På Tønsberg kommunens hjemmeside kan du gå inn på «Barnehage» og se etter «*Her kan du søke om barnehageplass*». Hvis du vil ha hjelp med å søke barnehageplass kan du komme til Åpen barnehage (åpent på mandag og onsdag fra 09.00-15.00), det er på Familiehuset i nærheten av togstasjonen. Adresse; Halfdan Wilhelmsens alle 2, 3116 Tønsberg

### HVA KOSTER DET?

- Hvis du har lav inntekt, kan du ha rett til å betale mindre for barnehageplassen.
- Hvis du har flere barn i barnehagen, har du rett til å betale mindre.